TANGAZO LA SERIKALI NA. 543 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA UVINZA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Uvinza ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Uvinza.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA UVINZA


MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA UVINZA

*Makadirio ya eneo:* Hekta 17071.02 au Kilometa za Mraba 170.71

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi iliyohifadhiwa awali chini ya Msitu wa Hifadhi Uvinza linalopatikana Wilaya ya Uvinza katika Mkoa wa Kigoma kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 3140 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatavyo:

*Tangao La Serikali Na. 543 (Linaendelea)*




Dodoma,
___24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*